AJIRA

# Madereva 470 wa Kitanzania wafaulu usaili wa ajira Qatar

**Na Imani Nathaniel**

ZAIDI ya madereva 470 wa Kitanzania wamefaulu usaili wa ajira Qatar, katika mpango maalum unaolenga kuwawezesha vijana wa Kitanzania kupata kazi katika sekta ya usafirishaji nje ya nchi.

Usaili huo unaofanyika katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Mabibo - Dar es Salaam, ulianza Mei 27 mwaka huu ukiwahusisha jumla ya madereva 800.

Katika awamu ya kwanza, madereva 477 wamefanikiwa kufuzu na tayari 103 wamepangiwa kuondoka kwa hatua ya mwanzo.

Kufikia Julai 28, 2025, madereva 28 kati ya hao walikuwa wamewasili salama Qatar. Wengine wanatarajiwa kuwasili kati ya Julai 29-30 na Agosti 1-3, 2028, huku waliobaki wakisubiri kukamilishiwa taratibu za viza na tiketi.

Mpango huu mkubwa unaendeshwa kwa ushirikiano wa karibu kati ya Kampuni ya Mowasalat (Karwa) ya Qatar, Wakala wa Ajira wa Tanzania na Qatar, na Ubalozi wa Tanzania nchini Qatar, chini ya uongozi wa Balozi Habibu Awesi Mohamed.

Mbali na ajira, Serikali ya Tanzania imepanga kutia

> Katika awamu ya kwanza, madereva 477 wamefanikiwa kufuzu na tayari 103 wamepangiwa kuondoka kwa hatua ya mwanzo.

saini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na Kampuni ya Karwa ili kuimarisha mafunzo katika maeneo ya udereva, ufundi na usafirishaji.

Makubaliano hayo yatahusisha taasisi mbalimbali ikiwamo NIT, VETA na Chuo cha Karume - Zanzibar.

Usaili huo unajumuisha vipengele vya mtihani wa nadharia na mtihani wa vitendo, ambapo waombaji hujaribiwa kuendesha magari barabarani ili kuthibitisha ujuzi wao wa udereva.

Serikali imeeleza kuwa mwitikio wa vijana umekuwa mkubwa, wengi wakijitokeza kwa hamasa kubwa na matumaini ya kupata fursa ya ajira nje ya nchi.

Kupitia mpango huu, serikali inatarajia kuongeza ajira kwa mamia ya Watanzania na kukuza uhusiano wa kiuchumi na kijamii kati ya Tanzania na Qatar.



Baadhi ya madereva 28 wa Kitanzania wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Hamad, Doha, nchini Qatar, mapema wiki hii. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

CamScanner

Nipashe Alhamisi July 31, 2025 pg 18

USAFIRI

# UDART yataja sababu kuchelewa ununuzi mabasi ya mwendokasi

**Na Salome Kitomari**

KAMPUNI ya Mabasi ya Mwendokasi (UDART), imesema kuchelewa kwa taratibu za ununuzi ndio sababu ya mabasi 99 kutowasili Agosti kama ilivyoelezwa awali, na sasa yataingia nchini kati ya Septemba mwishoni hadi Oktoba, mwaka huu.

Aidha, imewahakikishia watumiaji wa mwendokasi Dar es Salaam kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, amedhamiria kuwa ikifika Desemba, mwaka huu tatizo la usafiri linaondoka na njia zote sita zina mabasi ya kutosha kwa kadri ya mahitaji.

Akizungumza jana na wahariri na waandishi, Mkurugenzi Mtendaji wa UDART, Waziri Kindamba alisema mchakato wa ununuzi ulichelewa, lakini kwasasa kuna matumaini makubwa, kwa kuwa mabasi yameshakamilika na mambo machache yamebakia na kupakiwa kwenye meli kwa ajili ya kuja nchini.

Alisema UDART katika kuboresha utendaji kazi na uwajibikaji wanaishi kwenye falsafa mbili za Rais Samia, ambazo ni kujenga upya na mabadiliko ambayo wamejipa muda wa mwaka mmoja, kwa kuanza na kuhakikisha mabasi yanapatikana njia ya Kimara.

Kindamba alisema kampuni hiyo ilikuwa na ufisadi na ubadhilifu mkubwa, ikiwamo kutofanya matengenezo ya mabasi na kuyaacha yaingie maji ya mafuriko, wakati ingewezekana kuzuia.

"Hata baada ya kuingia mapato mengi yalikuwa yanapotea kutokana na watu kulipa kwa fedha taslimu, lakini tangu tuanzishe matumizi ya kadi. Tunawaomba wananchi watuvumilie kero ya usafiri itakuwa historia, mabasi tuliyonayo ni chakavu ambayo umri wake umeisha muda mrefu," alisema.

Aidha, alisema mabasi mapya yanatumia gesi na kwa basi moja la mfano wameona namna wanavyookoa fedha nyingi, na kwamba matumizi ya mafuta yalikuwa mzigo mzito kwa kampuni hiyo.

Pia, alisema kimsingi UDART inatoza nauli ndogo ikilinganishwa na nchi za Afrika zinazotoa huduma ya usafiri, na kwamba awali nauli ilipendekezwa kuwa Sh. 1,200, lakini serikali inajali wananchi wake ikapanga Sh. 650 na baadaye ilipanda hadi 750. "Serikali imedhamiria miradi mingine ya mwendokasi kuendeshwa kwa ushirikiano na sekta binafsi, tumeanza na njia ya Mbagala, tutaendelea kwenye njia nyingine ikiwamo kuongeza mabasi katika njia ya Kimara," alisema.

Kindamba alisema UDART imekipa Benki ya NMB kwa kuwa ununuzi wa mabasi ni bei kubwa na kwamba basi moja linauzwa Sh. milioni 500, na kwamba kama ambayo sekta binafsi inakopo na kuwekeza si jambo la ajabu kwa serikali kukopa kwa ajili ya kuboresha usafiri.

Aidha, alisema moja ya maboresho yaliyofanyika ni serikali kuondoa gharama za miundombinu ambazo walikuwa wanalipa Sh. milioni 27 kila siku, na sasa watalipa kwa asilimia jambo ambalo litakuwa nafuu.

Kuhusu kujiunga Soko la Hisa Dar es Salaam, alisema hawawezi kujiunga kutokana na kwamba hesabu zao hazikuwa safi,na kwamba kampuni inategeneza hasara hivyo lazima isafishe hesabu zake ndipo wajiunge kwenye huko.